

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA  
KURUGENZI YA MAWASILIANO YA RAIS, IKULU



*Dar es Salaam*  
*02 Mei, 2026*

Baruapepe: [press@ikulu.go.tz](mailto:press@ikulu.go.tz)

**TAARIFA KWA UMMA**  
**RAIS WA JAMHURI YA RWANDA KUFANYA**  
**ZIARA YA KIKAZI NCHINI**

Rais wa Jamhuri ya Rwanda, Mheshimiwa Paul Kagame anatarajiwa kuwasili nchini, kesho Jumapili, tarehe 03 Mei, 2026, kwa ziara ya kikazi ya siku moja.

Katika ziara hiyo, Rais Kagame atafanya mazungumzo na mwenyeji wake, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan.

Mazungumzo yao yataangazia masuala ya ushirikiano kati ya nchi hizo mbili.

Bakari S. Machumu

Mkurugenzi wa Mawasiliano ya Rais, Ikulu



[Ikulu Mawasiliano / ikulu\\_mawasiliano /](#)  
[ikulu\\_Tanzania / ikulu Tanzania /](#)  
[ikulumawasilano / Ikulu Tanzania / Ikulu Tanzania](#)

